TANGAZO LA SERIKALI Na. 63 la tarehe 31/1/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128(2))*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KATIKA KEMIKALI YA ETHANOL INAYOTUMIKA KUZALISHA LADHA ZA KAHAWA, KOKOA NA VANILA KWA KAMPUNI YA NATURAL EXTRACT INDUSTRIAL LIMITED YA MWAKA 2025

Jinan a kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa katika Kemikali ya Ethanol inayotumika katika Mradi wa Kuzalisha Ladha za Kahawa, Kokoa na Vanila kwa Kampuni ya Natural Extract Industrial Limited ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 2 Disemba, 2024.

Msamaha

**2**. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa bidhaa iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii inayoingizwa ndani au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na au kwa niaba ya Kampuni ya Natural Extract Industrial Limited kwa ajili ya kuzalisha ladha za Kahawa, Kokoa na Vanila unasamehewa.

Masharti

**3**. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa bidhaa itatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

**4**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 1 Disemba, 2025.

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | MAELEZO | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ethanol | Lita | 36,000 |

Dodoma,
17 Januari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*